## Q. Viroboto na kupe

- Mbwa akiwa na viroboto hujikuna mara kwa mara, hujing'ata sehemu za nyuma na hasa chini ya mkia. Baadhi ya mbwa hupata mzio (allergy) wanapokutana na mate ya viroboto, kwa hiyo wakiumwa na kiroboto hupata ugonjwa wa ngozi

- Mbwa akiwa na viroboto kwenye ngozi utaona wadudu wenye rangi ya kahawia wakitembea kwenye ngozi na manyoya. Au unaweza kuona uchafu mweusi ambao huonyesha kinyesi cha viroboto.

  Ili kudhibiti viroboto ni vema pia kuua viroboto kwenye mbwa na mazingira yake. Hii ni kwa sababu viroboto hutumia muda mwingi wa maisha yao nje ya mbwa. Safisha matandiko ya mbwa na tumia dawa za kuua wadudu kwenye mazingira.

  **Kupe** huleta maambukizi ya vimelea hatari kwa uhai wa mbwa. Mbwa aogeshwe kwa dawa za kuua kupe mara moja kwa wiki.

## 5. Kuondoa kizazi majike/Kuhasi madume

- Kama hutaki mbwa wako wazae muone Daktari wa mifugo akuelekeze jinsi ya kuzuia mbwa JIKE kushika mimba au jinsi ya hudhibiti MADUME

- Mbwa jike huingia kwenye joto kila baada ya miezi sita. Akiwa kwenye joto jike huvutia madume kumfuata ambayo huweza kusafiri umbali mrefu. hii husababisha matatizo kwako na kwa majirani na pia mbwa jike kupata mimba bila kutegemewa. Kuzuia uzaaji usiotakiwa mbwa jike hutolewa kizazi kwa operesheni kubwa. Hii inaweza hufanyika kwa mbwa wa kuanzia miezi tisa.

  Ili kudhibiti uzazi na uzururaji mbwa dume hufanyiwa operesheni ya kuhasi kuanzia anapofikisha miezi sita.

**WASILIANA NA KLINIKI JUU YA UTARATIBU NA GHARAMA ZA OPERESHENI HIZI**

## 6. Matunzo ya watoto wa mbwa

- Mbwa mdogo akiwa na umri wa wiki 4 hadi sita anatakiwa aanzishwe kupatiwa chakula cha ziada akiwa bado ananyonya ili aanze kukizoea taratibu.

- Mbwa mdogo akiisha fikia umri kati ya wiki 6 hadi 8 anaweza kuachishwa kunyonya maziwa ya mama; na akatunzwa mbali na mama yake.



## 7. Muda wa huduma

Jumatatu hadi Ijumaa
Saa 2 asubuhi hadi saa 9 na nusu jioni
Jumamosi
Saa 2 asubuhi hadi saa 6 mchana

***Imetolewa na***
***Kliniki ya Mifugo,***
***Kitivo cha Tiba ya Mifugo,***
***Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo,***
***P. O. Box 3015 Chuo Kikuu MOROGORO.***
***Simu: 0683-30 15 30 (Airtel)***

**SOKOINE UNIVERSITY OF AGRICULTURE**

**VETERINARY CLINIC**

# AFYA

# NA

# MATUNZO BORA YA MBWA WAKO



**YALIYOMO:**

1. Huduma ya kwanza
2. Chanjo za muhimu kwa mbwa
3. Kinga na tiba ya minyoo
4. Viroboto na kupe
5. Kuhasi na kuondoa vizazi
6. Matunzo ya mbwa watoto
7. Muda wa Huduma

## 1. Huduma ya kwanza

Kama wanyama wengine mbwa anaweza kujiumiza, hivyo ili kuweza kupunguza madhara mbali mbali yanayoweza hatarisha uhai wa mbwa zingatia yafuatayo:

- Daktari wa mifugo ni mtu muhimu sana anayeweza kusaidia kuzuia maumivu ya mbwa yasiendelee kuwa makubwa, hakikisha kuwa unafahamu hospitali ya wanyama na ufahamu taratibu za kazi na wakati wa dharura ujue utawapataje? (namba ya simu au mahali wanapoishi).
- Mojawapo ya mifano ambayo inaweza kusababisha mbwa akaumia na kuhitaji huduma ya kwanza ni ajali za barabarani, kukatwa na kitu, kuumwa na nyoka na madhara ya sumu. Sababu nyingine ambazo zinaweza kusababisha mbwa wako kuhitaji huduma ya kwanza ni magonjwa kama vile kuharisha na kutapika ghafla, kuzimia na kukabwa kitu kooni.
- Toa taarifa kwa Daktari wa mifugo mara tu mbwa wako akipata tatizo kabla ya kuchukua hatua yeyote.
- Mara nyingi inafaa umpeleke mbwa wako hospitali badala ya kutegemea Daktari kufika nyumbani kwako, kwa sababu anaweza akahitaji vifaa muhimu ambavyo viko hospitalini au akahitaji wasaidizi waliosomea fani ya tiba ya mifugo ambao wanapatikana hospitalini.



## 2. Chanjo

- Awali magonjwa hatari ya mbwa yanayosababishwa na virusi vya *parvo* na *distemper* yalisababisha vifo vingi kwa mbwa na hasa mbwa wenye umri mdogo; Upatikanaji chanjo kwa ajili ya magonjwa haya na mengineyo umepunguza sana vifo hivyo.
- Kuna tofauti katika utoaji wa chanjo kati ya nchi na nchi, na hata eneo kwa eneo hivyo ni vizuri uwasiliane na Daktari wa mifugo juu ya chanjo muhimu anazohitaji mbwa katika eneo lako.
- Chanjo humpatia mnyama wako kinga dhidi ya magonjwa. Pia tumia fursa ya kumpeleka mbwa hospitali kupima afya ya mbwa wako na kuuliza maswali kuhusu afya ya mbwa wako.
- Tahadhari ya pekee yapaswa kuchukuliwa juu ya kichaa cha mbwa. Kwa utaratibu wa nchi kila mbwa anapaswa kuchanjwa dhidi ya kichaa cha mbwa. Zingatia kwamba mbwa mwenye kichaa huuma binadamu na huweza kusababisha kifo ambacho huambatana na maumivu makali.

**PATA HUDUMA YA CHANJO JUMATATU HADI JUMAMOSI MUDA WA KAZI**



## 3. Kinga na tiba ya minyoo

- Tiba ya minyoo ni kitu muhimu sana kwa afya ya mbwa wako. Unatakiwa kumpatia mbwa wako tiba ya minyoo kwa mpangilio, na hasa ikiwa mbwa wako anakuwa karibu na watoto. Hii ni kwa sababu baadhi ya minyoo ya mbwa pia inaweza kuambukiza binadamu. Mbwa wakubwa wapewe dawa za minyoo kila
- Minyoo ya tegu ni tatizo kubwa katika mbwa, mbwa akiwa na minyoo ya aina hii utaona pingili za minyoo kwenye manyoya ya nyuma au kwenye kinyesi chake pingili hizi hufanana na punje za mchele na mara nyingi huonekana zikitembea.
- Unaweza ukaona pingili kubwa za minyoo hii ambazo huwa tambarare mithili ya utepe mweupe.
- Mbwa anaweza kupata minyoo ya tegu kwa kula nyama ya ng'ombe au mbuzi isiyopikwa. Aina nyingine ya tegu husambazwa na viroboto, ni vema kuzuia/kuua viroboto waliopo kwenye ngozi ya mbwa wako na mahali anapolala mara mbwa anaposhambuliwa na tegu.

Dawa za kawaida za michango haziuwi tegu, hii huhitaji dawa maalum za tegu, kuna dawa chache ambazo zinatibu minyoo aina ya tegu na michango. Pata ushauri toka kwa Daktari wa mifugo

**MBWA APEWE DAWA ZA MINYOO KILA BAADA YA MIEZI MITATU -MINYOO HUUA**

**Utaratibu wa kinga dhidi ya magonjwa ya mbwa**

| UGONJWA | MUDA WA KINGA /TIBA |
|---|---|
| **Kichaa cha mbwa (Rabies)** | **Umri wa miezi mitatu rudia mara moja kila mwaka** |
| **Kuharisha na kutapika damu (Parvovirus infection)** | Umri wa wiki 5-8, rudia kila baada ya wiki nne mpaka mbwa wako awe na wiki 16 rudia kila mwaka |
| **Distemper na Ugonjwa wa ini (Hepatitis)** | Umri wa wiki 5-8, rudia kila baada ya wiki 3 mpaka mbwa wako atakapo timiza umri wa wiki 13-15 rudia kila mwaka |
| **Homa ya manjano (Leptospirosis)** | Wiki 9 – 12 rudia kila mwaka |
| **Minyoo** | Umri wa wiki 6, halafu Kila baada ya miezi mitatu |